

## FORM 1 TERM 1 2021

### KISWAHILI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

(alama 10)

Malenga mlotukuka, kwa tungo zenu teule  
Tungo zenye kusifika, zenye na nasaha tele  
Naomba la uhakika, jawabu enyi wavyele  
Wa kuume tangu lini, kuukata wa kushoto !

Tangu dahari miaka, mikono ina upole  
'Meungana pasi shaka, ni miwili vile vile  
Mmoja ukisumbuka, mwingine hujaa ndwele  
Wa kuume tangu lini, kuukata wa kushoto !

Wa kuume ukicheka, wa kushoto nao vile  
Ulipofanya dhihaka, kwamba unao upele  
Wa kushoto hutanzuka, kuukuna kwa vidole  
Wa kuume tangu lini, kuukata wa kushoto !

Kimako leo amaka, kushoto haoni mbele  
Kumbe kuume kushika, kudhibiti mtale  
Misuli 'metutumuka, hajali hana simile  
Wa kuume tangu lini, kuukata wa kushoto !

Tamati ninaondoka, nawachia wakale  
Uamuzi wa haraka, ufanyike msilale  
Umenijaa wahaka, mwanzo wa ngoma ni lele  
Wa kuume tangu lini, kuukata wa kushoto !

#### **Mwaswali**

1. Shairi hili ni la aina gani? (Alama 1)
  
2. Eleza vina vya shairi hili. (Alama 2)
  
- 3 a) Mizani ni nini ? (Alama 1)
  
- b) Shairi hili lina mizani ngapi katika ubeti wa nne mshororo wa tatu ? (Alama 1)
  
4. Taja na ueleze maana ya kibwagizo cha shairi hili. (Alama 2)

5. Taja jambo ambalo hufanywa na mikono yote miwili kwa pamoja. (Alama 1)

6. Toa maana ya maneno haya kama yaliyotumiwa katika shairi. (Alama 2)

i) Dahari

ii) Kuume

### **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 20)**

a) Taja konsonanti ,mbili za ufizi. (Alama 2)

b) Taja irabu mbili za nyuma. (Alama 2)

c) Toa mifano mitatu ya ala tuli za kutamkia. (Alama 3)

d) Ni nini maana ya kiyeyusho/nusu – irabu ? (Alama 1)

e) Andika maneno mawili kwa kila mojawapo ya sauti hizi mwambatano. (Alama 2)

i) Nj

ii) Sw

f. i) Eleza maana ya silabi. (Alama 1)

ii) Onyesha silabi za neno parapanda. (Alama 2)

g) Taja aina moja ya kamusi. (Alama 1)

h) Mtu anayehudumu maktabani huitwaje ? (Alama 1)

i) Tambua aina za maneno katika sentensi hii. (Alama 2)  
Mtoto mtukutu ameadhibiwa vibaya.

j) Nomino hizi ziko katika ngeli gani ? (Alama 1)

i) Mkoba

ii) Ngao

k) Kamilisha methali hizi. (Alama 1)

i) Kikulacho .....

ii) Jambo usilolijua .....

l) Onyesha matumizi mawili ya nukta pacha/koloni. (Alama 1)